

Kusaidia ukuaji wa
lugha wa mtoto
anayezungumza
lugha nyingi

swahili

Ufasaha wa lugha mbili au lugha nyingi



- Ufasaha wa lugha mbili au lugha nyingi ni wa kawaida zaidi kuliko wa lugha moja.
- Ufasaha wa lugha nyingi hauongezi mwonekano wa matatizo ya ukuaji wa lugha.
- Hata hivyo, kukua ukiwa unazungumza lugha nyingi kunaweza kuhitaji muda na jitihada zaidi kutoka kwa wazazi.
- Inashauriwa kupanga chaguo la lugha mapema.
- Zungumza na mtoto kwa lugha unayoijua zaidi (mara nyingi lugha yako ya mama).
- Mtoto hujifunza Kifini katika kituo cha utunzaji wa mchana/shuleni.
 - Huna haja ya kuzungumza Kifini nyumbani.



Kusoma vitabu



- Kusoma pamoja huimarisha msamiati wa mtoto na stadi za mwingiliano.
- Chagua vitabu vyenye picha zinazowafaa watoto.
- Tumia picha kusimulia hadithi katika lugha yako mwenyewe (hata ikiwa maandishi katika kitabu hayako katika lugha yako mwenyewe).
- Taja picha hizo.
- Zungumza na mtoto wako kuhusu kile kilicho katika picha na kile kinachoendelea kwenye kitabu.
- Muulize mtoto alifikiria nini kuhusu hadithi hiyo.
- Hadithi ya wakati wa kulala inaweza kuwa njia nzuri ya kutulia ili kulala.
- Tembelea maktaba na mtoto wako.



Maisha ya kila siku ya pamoja na mfano wa watu wazima

- Mpe mtoto wako mfano.
 - Toa mfano wa majibu ya mtoto wako kwa lugha ya nyumbani, hata ikiwa atakujibu kwa lugha tofauti.
- Mtoto hujifunza lugha katika maisha ya kila siku.
 - Mshirikishe mtoto katika kazi za nyumbani (kwa mfano, kupika, kufanya usafi).
- Zungumza na mtoto wako.
- Mwambie mtoto unachofanya na kile anachofanya.
 - "Sasa ninaweka uma na visu mezani".
 - "Unaweza kuvalaa viatu vyako mwenyewe".
- Tumia majina halisi ya vitu.
 - Badala ya kusema "peleka hizi huko," jaribu kusema "peleka soksi hizi kwenye kikapu katika kabati lako la nguo."
- Mwombe mtoto wako akupe taarifa za kila siku. Mhimize mtoto wako akuambie kuhusu siku yake katika kituo cha utunzaji wa mchana/shuleni.
 - Unaweza kumsaidia mtoto wako kwa kuuliza maswali mahususi (nani, nini, wapi).
- Mtoto hujifunza kwa kucheza.
 - Cheza pamoja na mtoto ana kwa ana.
- Nyimbo na mashairi husaidia ukuzaji wa usemi na lugha.



Muda wa kutazama skrini

- Mtoto hujifunza kutumia lugha katika mwingiliano na watu wengine, si kupitia skrini.
- Skrini: televisheni, simu, kompyuta kibao na kompyuta
- Muda wa kutazama skrini uliopendekezwa:
 - Mtoto mwenye umri wa miaka 0–2 hahitaji skrini hata kidogo
 - Mtoto mwenye umri wa miaka 3–5 hadi saa 1 kwa siku
 - Mtoto mwenye umri wa zaidi ya miaka 6 hadi saa 2 kwa siku
- Mtoto anaweza kujifunza mambo kupitia skrini, lakini si bila ushiriki wa mtu mzima.
- Usichague Kiingereza kama lugha yako ya skrini ikiwa lugha yako ya nyumbani si Kiingereza.
- Pia zingatia muda wako wa kutazama skrini.



Taarifa zaidi

- Kliniki ya afya ya watoto
- Väestöliitto Hyvä kysymys - tovuti, Lapsi oppii - mfululizo
 - <https://www.hyvakysymys.fi/video/lapsi-oppii-monikielinen-perhe-vuorovaikutus-ja-kielen-oppiminen/>



**Kanta-Hämeen
hyvinvointialue**
Huduma za
urekebishaji kwa
watoto na vijana,
tiba ya usemi